# Fikiria

**na**

**Ellis P. Forsman**

# Fikiria

**na**

**Ellis P. Forsman**

**Octoba 11, 2011**

# Fikiria

## Ayubu 37:14

Fikiria kazi za ajabu za Mungu. Ayu. 37:14, "*Sikiliza neno hili Ee Ayubu; simama kimya uzifikiri kazi za Mungu za ajabu.*"

Anga. Zaburi 19:1, "*Mbingu zauhubiri utukufu wa Mungu, na anga laitangaza kazi za mikono yake.*"

Baraka zote. Yakobo 1:17, "*Kila kutoa kuliko kwema na kila kitolewacho kilicho kamili, hutoka juu hushuka kwa Baba wa mianga kwake hakuna kubadilika wala kivuli cha kugeuka geuka.*"

## Fikiria njia za chungu

Mit. 6:6, "Ewe mvivu mwendee chungu zitafakari njia zake upate hekima."

Biblia inafundisha uwanda. 2 Thes. 3:10, "*Kwa kuwa hata wakati ule tulipokuwa kwenu tuliwaagiza neon hili, kwamba ikiwa mtu hataki kufanya kazi, basi asile chakula.*"

Chungu ndiyo mfano. Efe. 4:28, "*Mwibaji asiibe tena; bali afadhali afanye juhudi, akitenda kazi iliyo nzuri kwa mikono yake mwenyewe, apate kuwa na kitu cha kumgawia mwenye kuhitaji.*"

**Tunafundishwa kufanya kazi pamoja.** Zab. 133:1, "*Tazama jinsi ilivyo vyema na kupendeza, ndugu wakae pamoja kwa umoja.*"

**Chungu hufanya maandalizi wakati wa hari**.

- Mit. 30:25, "*Chungu ni watu wasio na nguvu; lakini hujiwekea chakula wakati wa hari.*"
- Na tunapaswa kujiandaa ili kumpokea bwana harusi. Mat. 25:1-13, "*Ndipo ufalme wa mbinguni utakapo fanana na wanawali kumi waliotwaa taa zao, wakatoka kwenda kumlaki bwana arusi. Watano wao walikuwa wapumbavu, na watano wenye busara. Wale waliokuwa wapumbavu walizitwaa taa zao, wasitwae na mafuta pamoja nao; bali wale wenye busara walitwaa mafuta katika vyombo vyao pamoja na taa zao. Hata bwana arusi alipokawia, wote wakasinzia wakalala usingizi. Lakini usiku wa manane pakawa na kelele, haya bwana arusi tokeni mwende kumlaki. Mara wakaondoka wale wanawali wote, wakazitengeneza taa zao. Wale wapumbavu wakawaambia wenye busara, tupeni mafuta yenu kidogo; maana taa zetu zinazimika. Lakini wale wenye*

*busara wakawajibu, wakisema, sivyo hayatatutosha sisi na ninyi; afadhali shikeni njia mwende kwa wauzao mwende mkajinunulie. Na hao walipokuwa wakienda kununua, bwana arusi akaja, nao walio kuwa tayari wakaingia pamoja naye arusini; mlango ukafungwa. Halafu wakaja na wale wanawali wengine, wakasema Bwana, Bwana, utufungulie. Akajibu akasema, Amini, nawaambia, siwajui ninyi. Basi kesheni kwa sababu hamwijui siku wala saa.*"

## Fikiria Mungu anavyowajali ndege wa angani na majani ya kondeni

Mat. 6:25-30, "*Waangalieni ndege wa angani ya kwamba hawapandi, wala hawavuni, wala hawakusanyi ghalani na Baba yenu wa mbinguni huwalisha hao, ninyi je si bora kuliko hao? Ni yupi kati yenu ambaye akijisumbua aweza kujiongeza kimo chake hata mkono mmoja? Na mavazi ya nini kuyasumbukia? Fikirini maua ya mashamba jinsi yameavyo hayafanyi kazi, wala hayasokoti name nawaambia ya kwamba hata Sulemani katika fahari yake yote hakuvikwa vizuri kama moja wapo ya hayo. Basi ikiwa Mungu huwavika hivi majani ya kondeni, yaliyopo leo na kesho hutupwa kalibuni, je hatazidi sana kuwavika ninyi, enyi wa imani haba.*"

Mungu aliye na uwezo wa kuwalisha ndege wa angani na kuwavika majani ya kondeni, ana uwezo pia wa kulisha na kuwavika wanadamu.

# Mfikirie Kristo

Ebr. 12:3, "*Maana mtafakarini yeye aliyeyastahimili mapingamizi makubwa namna hii ya watendao dhambi juu ya nafsi zao, msije mkachoka mkizimia mioyoni mwenu.*"

Fikiria kile alichokistahimili (angalia msitari hapo juu). Fikiria yote aliyostahimili. Alifanya hivi kwa ajili yetu. Luka 19:10, "*Kwa kuwa Mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea.*" Mwelekeo huo ututia nguvu tusichoke na kuzimia mioyo (angalia Ebr. 12:3 hapo juu).

## Jifikirie Mwenyewe

Gal. 6:1, "*Ndugu mtu akighafilika katika kosa lo lote ninyi mlio wa Roho mrejezeni mtu kama huyo kwa roho ya upole, ukijiangalia nafsi yako usije ukajaribiwa wewe mwenyewe.*"

**Usije ukajaribiwa** (angalia msitari hapo juu).

Ujue udhaifu wako na ujitahidi kuachana nazo mwenyewe.

**Fikiria wito wako.** Efe. 4:1, "*Kwa hiyo nawasii mimi niliye mfungwa katika Bwana mwenende kama unavyoustahili wito wenu mlioitiwa;*"

**Fikiria thamani ya nafsi yako.** Mat. 16:26, "*Kwani atafaidiwa nini mtu akiupata ulimwengu wote na kupata hasara ya nafsi yake? Au mtu atatoa nini badala ya nafsi yake?*"

# Fikiria kila mmoja

Ebr. 10:24, "*Tukaangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana katika upendo na kazi nzuri.*"

**Kuhimizana katika upendo.** Tunapaswa kuwa watu wanaopenda. 1 Thes. 4:9, "*Katika habari ya upendano, hamna haja niwaandikie; maana ninyi wenyewe mmefundishwa na Mungu kupendana.*"

**Tunapaswa kusameheana.** Mat. 6:12-15, "*Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasameheavyo wadeni wetu. Na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu. Kwa kuwa ufalme ni wako na nguvu na utukufu hata milele. Amina. Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi. Bali msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu.*"

**Tunapaswa kuwa wavumilivu.** Efe. 4:2, "*Kwa unyenyekevu wote na upole, kwa uvumilivu, mkichukuliana kwa upendo.*"

**Hatupaswi kuwa wabinafsi.**

- Fil. 2:4, "*Kila mtu asiangalie mambo yake mwenyewe, bali kila mtu aangalie mambo ya wengine.*"
- Yak.2:15-16, "*Ikiwa ndugu mwanamume au ndugu mwanamke yu uchi na kupungukiwa na riziki, na mtu wa kwenu akawaambia enendeni zenu kwa amani mkaote mto na kushiba, lakini asiwape mahitaji yafaa nini?*"
- Ebr. 13:1-2, "*Upendano wa ndugu. Msisahau kuwafadhili wageni; maana kwa njia hii wengine wamewakaribisha malaika pasipo kujua.*"

**Kuhimizana katika kazi njema.** Kuhimiza kila mmoja katika kazi njema. Lazima kuwe na ukarimu na kujali sehemu ya mwili wa Kristo kila mmoja. 1 Kor. 12:25, "*Ili kusiwe na faraka katika mwili, bali viungo vitunzane kila kiungo na mwenziwe.*"

**Kuwahudumia wengine kama wewe unavyotaka uhudumiwe.** Mat. 7:12, "*Basi yo yote mtakayo mtendewe na watu nanyi watendeeni vivyo hivyo; maana hivyo ndivyo torati na manabii.*"

**Kubeba mizigo yao.**

- Gal. 6:1, "*Ndugu zangu mtu akighafilika katika kosa lo lote, ninyi mlio wa Roho mrejezeni huyo mtu kama huyo kwa roho ya upole, ukijiangalia nafsi yako usije ukajaribiwa wewe mwenyewe.*"
- Rum. 12:15, "*Furahini pamoja nao wafurahio; lieni pamoja nao waliao.*"

**Kuwa waangalizi wao.**

- Mwanzo 4:9, "*BWANA akamwambia Kaini, yuko wapi Habili ndugu yako? Akasema sijui, mimi ni mlinzi wa ndugu yangu?*"
- Luka 10:29-37, "*Naye akitaka kudai haki, alimwuliza Yesu, na jirani yangu ni nani? Yesu akajibu akasema, mtu mmoja alishuka toka Yerusalemu kwenda Yeriko, akaangukia kati ya wanyang'anyi; wakamvua nguo, wakamtia jeraha wakaenda zao, wakimwacha karibu ya kufa. Kwa nasibu kuhani mmoja alishuka kwa njia ile; na alipomwona alipita kando. Na Mlawi vivyo hivyo, alipofika pale akamwona akapita kando. Lakini Msamaria mmoja katika kusafiri kwake alifika hapo alipo, na alipomwona alimhurumia, akakaribia, akamfunga jeraha zake akizitia mafuta na divai; akampandisha juu ya mnyama wake, akampeleka mpaka nyumba ya wageni akamtunza. Hata siku ya pili akatoa dinari mbili akampa mwenye nyumba ya wageni, akisema mtunze huyu na cho chote utakachogharimiwa zaidi, mimi nitakaporudi nitakulipa. Waonaje wewe katika hao watatu ni yupi aliyekuwa jirani yake yule aliyeangukia kati ya wanyang'anyi? Akasema ni huyo aliyemwonea huruma. Yesu akamwambia enenda zako, nawe ukafanye vivyo hivyo.*"
- Mat. 28:19-20, "*Basi enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Matakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.*"
- 1 Thes. 4:1, "*Iliyobaki ndugu tunakusihini na kuwaonya kwamba mwenende katika Bwana Yesu; kama mlivyopokea kwetu jinsi iwapasavyo kuenenda na kumpendeza Mungu, kama ninyi mnavyoenenda, vivyo hivyo mpate kuzidi sana.*"